

**MAAKIZO.**

**KIDATO CHA KWANZA.**

**1. UFAHAMU (ALAMA 10)**

**Maswali**

- a) Taja sehemu tatu ambako kawi ya umeme hutumiwa. (ala 3)
- i. Nyumbani**
  - ii. Viwandani**
  - iii. Asasi mbalimbali.**
- b) Eleza changamoto inayoikumba nchi inayotegemea maji kama chanzo cha kawi. (ala 1)
- Mvua isiyotabirika.**
- c) Mbali na maji, taja vyanzo vingine vya kawi. (ala 3)
- **Jua**
  - **Mvuke**
  - **Upepo**
- d) Kwa mujibu wa taarifa, andika matumizi matatu ya kawi ya upepo. (ala 3)
- **Kuendeshea mitambo ya;**
  - **Kusaga nafaka**
  - **Kupasulia mbao**
  - **Kutolea maji visimani.**

**SARUFI (ALAMA 15)**

1. Tofautisha kati ya irabu na konsonanti. (ala 2)
- Irabu ni sauti ambazo hutamkwa kwa ulaini bila ya hewa kuzuiliwa.**
2. Taja sifa bainifu za irabu zifuatazo. (ala 2)
- a) /o/ - **Ni irabu ya nyuma chini. ( ½ al)**  
**Inapotamkwa midomo huviringwa ( ½ al)**
- b) /e/ - **Ni irabu ya mbele chini ( ½ )**  
**Inapotamkwa midomo hutandazika ( ½ )**
3. Tofautisha kati ya sauti ghuna na sauti sikhuna. (ala 2)
- Sauti ghuna ni sauti ambazo zinapotamkwa husababisha mrindimo wa nyuzi za sauti.**  
**Sauti sikhuna zinapotamkwa hazisababishi mrindimo wa nyuzi za sauti.**
4. Taja vipashio vya lugha. (ala 2)
- Sauti → Silabi → Neno → Sentensi**

5. Andika kwa wingi (ala 1)  
Mtoto mvulana angali anacheza kandanda.  
**Watoto wavulana wangali wanacheza kandanda.**
6. Andika neno lenye mpangilio ufuatao wa silabi. (ala 2)  
(a) KKKI **mf. Mchele, mbwa.**  
(b) KKI **mf. Mti, mtoto.**
7. Bainisha aina za maneno katika sentensi ifuatayo. (ala 2)  
Mwanafunzi mrefu anavuka barabara.  
**N V T N**
8. Tofautisha kati ya ala tuli na ala songezi na utolee mifano. (ala 2)  
**Ala tuli hazisogeisogei wakati wa kutamka sauti mf. Kaakaa gumu, kaakaa laini**  
**Ala sogezi husogeasogea wakati wa kutamka sauti mf. Ulimi, mdomo,**

**ISIMU JAMII (ALAMA 5)**

- i. Ni nini maana ya Isimu Jamii. (ala 1)  
**Isimu Jamii ni sayansi inayochunguza uhusiano uliopo kati ya lugha na jamii.**
- ii. Eleza maana ya sajili / Regista. (ala 1)  
**Sajili ya lugha ni matumizi ya lugha katika muktadha maalum/mahususi.**
- iii. Taja kaida zozote tatu za lugha. (ala 3)  
- **Umri**  
- **Wahusika**  
- **Tabaka**  
- **Wakati** (alama 1 kila moja.)